UTAYARISHAJI WA IKAMA NA BAJETI YA MISHAHARA KUPITIA MFUMO WA TAARIFA ZA KIUTUMISHI NA MISHAHARA (HCMIS) KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

UTANGULIZI

- Mtakumbuka kwamba kwa mujibu wa kifungu Na. 8 (2) (d) na 3 (b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kikisomwa kwa pamoja na Hati ya Mgawanyo wa Majukumu (instrument) iliyotolewa kwenye Gazeti la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba, 2010 imetamkwa kuwa nanukuu ***"Subject to any specific or general direction, of Chief Secretary, the Permanent Secretary Establishment shall …… carryout a review of annual personnel emolument to ensure that personnel emoluments expenditure conforms to budget ceillings" mwisho wa kunukuu. Kama mtakavyoona hapa Katibu Mkuu Utumishi ndiye msimamizi mkuu wa Ikama na bajeti ya mshahara ya watumishi wa umma katika:-***

UTANGULIZI…

- Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea,
- Sekretarieti za Mikoa,
- Halmashauri za Serikali za Mitaa,
- Wakala wa serikali,
- Taasisi za Umma ambazo zinapata ruzuku ya mshahara kwa asilimia 100%
- Hospitali za mashirika ya kujitegemea (VAH), hospitali Teule za wilaya (DDH)

MAMBO YALIYOPASWA KUZINGATIWA KATIKA IKAMA NA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

- Kuzingatia maelekezo ya mwongozo wa matayarisho ya bajeti ya serikali (budget guideline) kwa kuhakikisha kwamba kila mwajiri havuki ukomo wa bajeti uliowekwa,

- Kuzingatia maeneo ya vipaumbele na yenye Matokeo Makubwa sasa kama Elimu, Afya, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Gesi asilia, Misitu na Wanyamapori

- Kuzingatia kuwepo kwa taarifa sahihi za kiutumishi katika Mfumo wa HCMIS na kuutumia mfumo huo kufanya makisio

- Mapendekezo ya kupandisha watumishi vyeo yazingatie kuwepo kwa taarifa za upimaji utendaji kazi kwa uwazi (OPRAS)

- Sekretariet za Mikoa zitoe msaada wa kiufundi kwa Halmashauri za serikali za mitaa zilizopo ndani ya mkoa husika

MAPITIO YA IKAMA NA BAJETI YA MSHAHARA KWA MWAKA 2014/2015.

- Zoezi la kutayarisha makisio ya Ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 lilifanyika kupitia Mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS). Utayarishaji wa makisio ya Ikama na bajeti ulifanyika baada ya kuwepo kwa hatua za kusafisha taarifa za kiutumishi na mishahara kupitia Mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS). Uandaaji wa Ikama na mishahara kwenye mfumo wa HCMIS yaliwezesha kuwasilisha Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma mahitaji yao ya Ikama kwa mwaka 2014/2015 bila kulazimika kwa Maafisa wanaoshughulikia makisio ya Ikama kusafiri kuja Dar es Salaam.

FAIDA ZA KUANDAA IKAMA NA BAJETI YA MSHAHARA

- Kuhakikisha kwamba serikali inao watumishi wa kutosha na wenye taaluma, ujuzi na uzoefu wa kutosha kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma kwa wananchi wake kwa lengo la kufikia malengo yake,
- Kuhakikisha kwamba watumishi wa ziada waliopo wanapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu kulingana na mahitaji ya mwajiri,
- Kuhakikisha kwamba mahitaji mapya ya watumishi yanaendana na vipaumbele vya Taifa na kwamba mahitaji hayo hayasababishi kuvuka kwa bajeti ya mshahara iliyotengwa katika mwaka wa fedha unaohusika,
- Kuhakikisha kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia masuala ya matumizi bora ya rasilimali watu na malipo ya mshahara zinatekelezwa ipasavyo.

CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UANDAAJI WA MAKISIO YA IKAMA NA MISHAHARA 2014/2015

- (i)Waajiri kuomba kuajiri idadi kubwa ya watumishi hawapatikani kutoka kwenye soko la ajira.
- (ii) Waajiri kutozingatia uzito wa majukumu ya kutekeleza (work load) hivyo kusababisha watumishi walioko vituoni kutokuwa na majukumu ya kutosha.
- (iii) Ikama kwa baadhi ya nafasi haikuzingatia vipaumbele vya Taasisi husika na hasa ikizingatiwa kuwa katika hali ya Bajeti finyu ajira inapaswa kuelekezwa katika utelekezaji wa majukumu ya msingi (core functions).
- (iv) Nafasi zilizopendekezwa kwa ajili ya upandishwaji vyeo ziliombwa kama ajira mpya badala ya kuombwa kama nafasi za uteuzi au kupandishwa vyeo.

CHANGAMOTO …

- (v) Waajiri kuwasilisha maombi yaliyozingatia dhana iliyokuwepo hapo awali kwamba ni vyema kuwasilisha idadi kubwa ya Ikama ili ikipunguzwa zibakie nafasi za kutosha.

- Waajiri kutokamilisha zoezi la kusafisha taarifa za kiutumishi na mshahara kwenye mfumo wa HCMIS

- (vii) Waajiri kuendelea na utaratibu wa kuwalipa mishahara watumishi nje ya “payroll” ya Serikali
- (viii) Baadhi ya nafasi za Ikama zilizoombwa kutozingatia viwango vya mshahara vilivyoidhinishwa katika miundo ya Utumishi.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MAKISIO YA IKAMA 2015/2016

- Kuandaa mipango madhubuti ya rasilimaliwatu kulingana na mahitaji halisi ya waajiri kwa kuwa makisio haya yanachukua zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya pato la taifa.

- (ii) Sekta zilizopo katika utekelezaji wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now –BRN) zipewe kipaumbele kwa kuwa hii ni agenda ya kitaifa kwa sasa.

- (iii) Matumizi sahihi ya rasilimali za nchi yazingatiwe katika uandaaji wa makisio ikizingatiwa kwamba sekta ya utumishi wa umma inakua kwa kasi kubwa. Kwa mfano hadi tarehe 10/11/2014 serikali ilikuwa na jumla ya watumishi 517,459 kama inavyoonekana katika jedwali

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MAKISIO YA IKAMA 2015/2016

Na.	Mwajiri	Idadi ya watumishi	Asilimia ya wote
1	Wizara	23,605	4,56%
2	Sekretariet za Mikoa	11,892	2.30%
3	Idara zinazojitegemea	74,016	14.30%
4	Halmashauri za serikali za Mitaa	370,677	71.63
5	Vyuo Vikuu	9,821	1.90%
6	Wakala	12,777	2.30%
7	Taasisi za Umma	14,671	2.845
	JUMLA	**517,459**	**100%**

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA MAKISIO YA IKAMA 2015/2016

- Ajira ambazo sio za kipaumbele (*core function) za waajiri kama vile wahudumu wa Ofisi na walinzi zijazwe kwa utaratibu wa kuishirikisha sekta binafsi (PSP).*

- (v) Waajiri watoe maelezo bayana kuhusu sababu za maombi ya nafasi za ajira mpya kwa kila Ikama ya ziada inayoombwa.

- (vi) Waajiri wazingatie sifa za muundo wa kada husika kabla ya kutenga bajeti ya Ikama na mishahara kwa watumishi wanaobadilishiwa vyeo (Recategorization)

- (vii) Watumishi wote ambao wametimiza sifa za kupandishwa vyeo waingizwe kwenye makisio ili kuepuka malalamiko wakati zoezi la kuwapandisha watumishi vyeo

MWISHO

- Waajiri wote mnatakiwa kuzingatia utaratibu huu wa uandaaji Ikama na bajeti ya mishahara kupitia HCMIS. Aidha zoezi la uandaaji wa Ikama litafanyika kuanzia tarehe 15 Novemba hadi tarehe 30 Desemba 2014 hivyo waajiri wanakumbushwa kuhakikisha kuwa maafisa wenye dhamana ya kuandaa makisio ya Ikama na mishahara wanatekeleza kwa ufanisi jukumu hili muhimu.